## MAOMBI

### TAFADHALI WANA-HCF WOTE TUOMBEE MAMBO YAFUATAYO:

***Kamati ya Maandalizi:*** Umoja, ushirikiano, kujituma na kutiana moyo, n.k.; ***Wanenaji na Masomo:*** Mungu awatumie kutimiza makusudi yake mema; ***Walengwa:*** Tanzania nzima waitikie mwito kwa vitendo na kwa kishindo; ***Mkoa wa Arusha:*** Anga lifunguke kwa kazi ya Mungu kupitia HCF; ***Ruhusa:*** Kutoka mamlaka zote husika, Sehemu za kazi na Familia na Penginepo; ***Fedha:*** Upatikanaji wa ada ya Kongamano, fedha kwa familia, Nauli; ***Ombea pia Afya njema*** kwa wote (wanenaji, walengwa na familia/ ndugu/ jamaa zao; ***Ulinzi:*** usalama na amani mahali pote (nyumbani, kazini, njiani/ safarini); ***Mahali pa Kongamano:*** Malazi, chakula, ukumbi wa Kongamano, mazingira; ***Mipango mingine yote:*** Ratiba, vyombo vya mawasiliano; ***Kuombea Taifa la Tanzania*** na Viongozi wa Serikali na Mashirika ya Umma, na yale ya Binafsi na Kidini; ***Kuombea majirani*** zetu (nchi-nane zinazotuzunguka) na dunia nzima (mabara saba); ***Kuombea Taifa la Israeli*** na amani ya Yerusalemu; Kuomba Mungu aingilie kati mahali pote penye vita na kuleta amani; ***Kanisa lihubiri habari njema*** za injili ulimwenguni kote, Kuombea Wakristo wanaoteswa, Yatima, Wajane, na Watoto walio katika mazingira yenye changamoto; ***Mwisho:*** Ombea Yote yatakayojitokeza mbeleni kama Roho Mtakatifu atakavyokufunulia.

## KAMATI YA MAANDALIZI:
## KONGAMANO LA TAIFA LA HCF(T) - 2025 ARUSHA

**Mwenyekiti:** Dkt. Catherine M. Mung'ong'o, 0784510067, 0763410067
**Mratibu wa HCF - Arusha:** Ndg. Verynice Chitenje, 0785239345
**Mratibu Msaidizi:** Ndg. Grace Madimilo, 0786795973
**Mlezi:** Ndg. Anna Maimu, 0754555519
**Mwenyekiti Msaidizi:** Ndg. Godbless D. Massawe, 0754454120
**Katibu:** Ndg. Mwinjilisti Salome Stanley, 0653903061,
**Katibu Msaidizi:** Dkt. Eric Mbelle, 0677662827
**Mhazini:** Dkt. Anjela Aloyce Assey, 0787511406
**Mhazini Msaidizi:**
Ndg.Mwinjilisti Grace W. Macha, 0783778989
**Mratibu, Kanda Kaskazini:**
Ndg, Tegemea Kasuga 0745019262

**WAJUMBE:**

Dkt. Alex Ernest, 0674434225
Dkt. Noel Malya, 0696074500
Ndg.DNO: Niwaeli Sumari, 0713007687
Dkt. Eunice Minja, 0784321702
Ndg. Dainess Mangowi 0753989791
Ndg. Anjela Mhitu-0754440118
Dkt. Bujuku Emmanuel, 0754-693325
Ndg. Witness Kirenga, 0684464686
Ndg.Beatrice Mdoe, 0713667775
Dkt Samson Isaay, 0765100007
Dkt Rose Mende, 0757143412
Ndg. Josephine Bitesigwa 0784430892
Ndg. Sarah Loya, 0755971459
Ndg. Sophia Mushi, 0655292255
Ndg. Sadiki Temu, 0754867379
Dkt.Noeli Malya, 0696074500
Ndg. Martha Shayo, 0754913940
Dkt. Samwel Isaya, 0756471677
Ndg. Martha Sima, 0762-830819
Ndg. Doreen Mollel, 0761430626
Dkt.Fortunate Makoi, 0753162246
Ndg.Winny Mbawile 0762775844
Ndg. Ruth Kanana, 0782128422
Ndg. Helen Elias, 0756-448477
Ndg. Flora Kessy, 0788-670470
Ndg. Cecylia Alex, 0762-960297
Ndg. Joyce Kiango, 0754-835594
Ndg. Elizabeth Mashika, 0786282440
Ndg. Kaseko Kisula, 0764789810
Dkt. George Kopwe, 0783999841
Ndg.Eli Mrema, 0756979233
Ndg. Elizabeth Kopwe, 0745811398
Dkt. Flora Mritta 0689027578
Dkt. Amos Mwasamwanja, 0767386817
Ndg. Maritha Shayo, 0754913940
Ndg. Twilumba Nkwama, 0763872145
Ndg. Salome Usallu, 0763715779
Dkt. Alex Mremi, 0717083983

## KWA KUJIANDIKISHA,

Jaza fomu hii na weka fedha katika akaunti ya **HCF Benki ya NMB: Akaunti Na: 20906600029,** NMB Tawi la Muhimbili, Jina la Akaunti: Healthcare Christian Fellowship (HCF) Tanzania.

**NB.:** Baada ya Kuweka Fedha Benki, Tafadhali Tuma Kwa Mtunza Hazina SMS Yenye Jina Lako Kamili, Kituo Chako Cha Kazi, Jumla ya Fedha ulizotuma na Jina La Benki (NMB).

## KWA MAWASILIANO ZAIDI NA UONGOZI, MAKAO MAKUU - HCF TANZANIA

C/o Africa Evangelistic Enterprise (AEE) Building, C/o P.O.Box 10055, Dar-es-Salaam. Mahali: Kinondoni-B, Morrocco-Rd/ Msisiri-B Str. Hse. No.58.; Baada ya Makao Makuu, Mahakama ya Wilaya, Kinondoni.

M/Kiti: Dkt. Elifuraha Mumghamba (Simu: 0788-422245)
Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS), S.L.P. 65014, DSM.
Barua-pepe: emumghamba@gmail.com

Makamu M/Kiti: Ndg. Dkt. Isaac Makanda (Simu: 0788-415584),
Chuo Kikuu cha Kumbukumbu cha Hubert Kairuki (HKMU), S.L.P. 65300, DSM.
Barua-pepe: isaacbya@yahoo.com

Katibu: Ndg. Harvest Mariki (Simu: 0754-855654 / 0713-608691),
Chuo Kikuu Muhimbili (MUHAS), S.L.P. 65001, DSM.
Barua-pepe: bwanaasifiwe73@gmail.com

Mtunza Hazina: Ndg. Godwin Magwira, (Simu: 0789-103391)
Hospitali ya Taifa, Muhimbili, DSM.
Barua-pepe: godwin.magwira@gmail.com

Mratibu: Bi. Maria S. Singano-Jalas,
Simu: 0769-112540, 0689-377861 na 0655-616886;
Barua-Pepe: hcftanzania@gmail.com

F: BROCHURE HCF(2025) Arusha REM-v3a-OK (23.04.25 T14.09pm).

# KONGAMANO LA-25 HCF TANZANIA, ARUSHA
# SEPTEMBA 25-29, 2025.

Healthcare Christian Fellowship (HCF) Tanzania
"Ushirika wa Kikristo Katika Huduma za Afya Tanzania"
(Reg.No.S.A.14631)
Tovuti: http://www.hcftanzania.info/

**TWENDENI ARUSHA!**

**TUKALISIKIE NENO, AMBALO BWANA AMETUITIA !**





TUTAKUWA HAPA ARUSHA LUTHERAN MEDICAL CENTRE (ALMC)


RAIS WA HUDUMA YA HCF ULIMWENGUNI (HCF-INTERNATIONAL) DR. CHRIS STEYN AKIWA KWENYE PICHA YA PAMOJA NA WANACHAMA WA HCF TANZANIA.

*"Niite, Nami Nitakuitikia, Nami Nitakuonyesha Mambo Makubwa, Magumu, Usiyoyajua." (Yer. 33:3)"*

***Je?, Unajua Ukweli Huu Kuwa; "Watu Wengi Zaidi Hupita Hospitalini Kuliko Makanisani ?!"***





## KONGAMANO LA-25, HCF TANZANIA, ARUSHA LUTHERAN MEDICAL CENTRE (ALMC) (SEPTEMBA 25-29, 2025)

Mpendwa ...............................................................................

Ninakusalimu katika Jina la Yesu Kristo, Bwana na Mwokozi wetu. Ninakukaribisha sana kwenye Kongamano la-25 la "Healthcare Christian Fellowship (HCF) yaani Ushirika wa Kikristo Katika Huduma za Afya, Tanzania litakalofanyika Arusha, Hospitali ya Arusha Lutheran Medical Centre (ALMC) mnamo Septemba 25-29, 2025. Hii ni mara ya kwanza kwa Kongamano la HCF kitaifa kufanyika Arusha. Unakaribishwa sana.

### HCF NI NINI?

HCF ni Ushirika wa Wakristo wanaofanya kazi katika sekta ya afya ulimwenguni kote ambao wanamwamini na kumkiri Yesu Kristo kuwa ni Bwana na Mwokozi wa maisha yao binafsi. Ushirika huu sio Kanisa bali hufanya kazi kama mkono wa makanisa ili kutimiza Agizo Kuu la Mungu la kuihubiri Injili ya Yesu Kristo kwa watu wote ikiwa ni pamoja na wagonjwa tunaowahudumia, ndugu na jamaa zao na wafanyakazi wenzetu (Mk 16:15).

### MADA KUU

***"Niite, nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa,magumu usiyoyajua" (Yer. 33:3)".***

**MADA ZINGINE NI;** Haki huinua Taifa, bali dhambi ni aibu ya watu wo wote; Kumtegemea Roho Mtakatifu katika Changamoto za maisha ya sasa; Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea, Nitakushauri, jicho langu likikutazama; Mkristo na ujasiriamali siku za mwisho; Historia fupi ya HCFI na HCF Tanzania; Somo la "Saline" (Mbinu za kumshuhudia Yesu Kristo kwa watu).

**KUFUNGUA na KUFUNGA KONGAMANO:** Kongamano la 25 la HCF(T) Tunatarajia litafunguliwa na Uongozi wa juu wa Serikali, Mkoa wa ARUSHA. BWANA akitujalia, Kongamano litafungwa na Askofu mpakwa mafuta wa BWANA atakayeteuliwa na Kamati ya Maandalizi.

### MNENAJI WA MADA KUU NA WALIMU WA MADA ZILIZOTAJWA

Mnenaji wa Neno Kuu la Kongamano atakuwa Askofu David Nkone (Pentekoste, DSM). Watoa mada wengine ni Watumishi wa Mungu kutoka madhehebu mbalimbali ya Kikristo na Viongozi wa HCF(T).

**WALENGWA: TUNAWAKARIBISHA SANA -** Wafanyakazi Wakristo wote wa kada na ngazi zote katika Sekta ya Afya, Wachungaji na Wakristo binafsi wanaohudumia wagonjwa hospitalini na wapendwa wanaochangia huduma ya HCF Tanzania mnakaribishwa sana.

**USAFIRI:** "Arusha inafikika kwa mabasi na ndege pia. Usafiri kwenda Hosteli ya "Kwa Father Babu" ni rahisi sana, simu yao ni: (0743000611). Wasiliana na kamati ya usafiri kwa namba; (0677662827, 0787511406). Hospitali ya Arusha Lutheran Medical Centre (ALMC) iko katikati ya mji, karibu na Stendi ya zamani ya mabasi Arusha.



*Askofu David Nkone Huyu ndiye mnenaji wa Kongamano letu la 25, litakalofanyika ""ALMC, Arusha."*



## GHARAMA ZA KONGAMANO LA 25, HCF (2025) ARUSHA, ALMC HOSPITAL

### WAJUMBE WA KULALA

Kutokana na mazingira na ratiba, Wajumbe wote kutoka nje na ndani ya Arusha ingebariki sana kama wote wangelala mahali palipoandaliwa na Kamati ya Kongamano. Kila mjumbe wa kulala atalipa **Tshs.195,000/-** tu (ambayo ni Ada ya kujiandikisha kwenye Kongamano, Malazi ya siku nne "4 nights", Chakula na viburudisho kwa siku zote za Kongamano). Wajumbe watakaolala makwao watalipa **Tshs.162,000/-** tu (Ada ya kujiandikisha kwenye Kongamano, Chakula na viburudisho kwa siku zote za Kongamano.*Angalizo*:Wajumbe watakaokuja na watoto wa umri zaidi ya miaka-2 itawalazimu kuchangia kiasi cha **Tshs. 85,000/-** tu kwa gharama ya chakula na malazi.

***Gharama za Kongamano* tangu 2022 zimeongezeka kwa sababu** tunalazimika kuchangia matumizi ya ofisi, Makao Makuu-HCF(T) yaani Vitendea kazi, Gharama ya kupanga ofisi, (Jengo la AEE), Umeme, Maji, Ulinzi pamoja na mshahara wa Mratibu.

### WAGENI KUTOKA NJE YA TANZANIA:

Wageni watalipa gharama za Kongamano kwa fedha ya Tanzania.

### TUNAOMBA MCHANGO WAKO WA HALI NA MALI

Kulingana na neema ya Mungu jinsi alivyokujalia tunakukaribisha kushiriki kwa kumwezesha mjumbe mmoja au zaidi kutoka mkoa wowote kwa nia ya kuendeleza upendo wa ndugu. Waweza kuchangia ada yote ya Kongamano (Tshs.195,000/-) au nusu = 97,500/-, theluthi = 65,000/-, robo = 48,750/- au kiasi cho chote utakachoguswa kutoa. Tafadhali tuma: Kwa benki ya NMB, Akaunti ya HCF, Au kwa simu ya Mhazini (Zote zimeandikwa hapa nyuma).

### SHUKRANI KWA WANA-HCF na WAFADHILI WOTE

Tunawashukuru sana Wanachama wote, Washiriki binafsi, Marafiki wa HCF Tanzania na Makanisa mbalimbali, ambao kwa moyo wa kupenda mmekuwa/ mtakuwa tayari kuchangia gharama kwa wajumbe wa Kongamano hili la aina yake. Kwa miaka ishirini na mitano (25) sasa ndio mara ya kwanza na ya kihistoria kwamba kongamano letu litafanyika Arusha ALMC, ambapo Rais wa Huduma hii ulimwenguni (HCF-International") Dr. Chris Steyn aliwahi kupatembelea mnamo Juni 19, 2023 (walipokuwa wamekuja AICC kwenye Kongamano la Madaktari duniani (ICMDA).

### LUGHA KATIKA MKUTANO

Lugha ya Taifa ndiyo itakayotumika. Wageni watakaokuwa hawaelewi Kiswahili watahudumiwa kwa utaratibu maalum.

### VITU VYA KUJA NAVYO BINAFSI NA HALI YA HEWA

Kila mjumbe anashauriwa kuja na Biblia, Notebook, Kalamu, mswaki, dawa ya meno, ndala na nguo za baridi, sweta. Utabiri wa hali ya hewa Arusha, Septemba 25-29, 2025: **Joto Juu: 28ºC na Joto Chini: 15ºC** (baridi kiasi). Kwa waliotoka sehemu za joto, wajiandae vizuri.

## FOMU YA KUJIANDIKISHA KUHUDHURIA KONGAMANO LA 25, HCF TANZANIA (2025), ARUSHA, (SEPTEMBA 25 - 29,2025)

Fomu hii inapatikana hapa: http://www.hcftanzania.info/. Tafadhali jaza taarifa zako katika kipande hiki, kisha uzitume kwa sms au whatsapp kwa katibu (Ndg. H. Mariki, 0754-855654), Barua-Pepe: bwanaasifiwe73@gmail.com; hcftanzania@gmail.com

Jina la Ukoo: ...

Jina la Kwanza na Kati: ...

Jinsia:Mwanamume(...) / Mwanamke(...)

Umri (weka ( ✓ ), miaka: 20-24 [ ] , 25-29 [ ] , 30-34 [ ] , 35-39 [ ] , 40-44 [ ] , 45-49 [ ] , 50-54 [ ] , 55-59 [ ] , 60+ [ ]

Anuani ya Posta: ...

Simu zako: ... /...

Namba ya whatsapp: ...

Barua pepe (E-mail) : ...

Kazi yako na wadhifa wako: .../...

Dhehebu/Kanisa: ...

Tarehe ya kufika ARUSHA: ...Saa: ...

Tarehe ya kuondoka ARUSHA ...Saa: ...

Taarifa ya ziada /...

Mlemavu...

**Kumbuka:** BWANA akitujalia, Wajumbe watapokelewa Arusha (Hosteli ya kwa Father Babu, siku ya **Alhamisi jioni tarehe 25.9.2025.** Kongamano litafunguliwa Ijumaa katika Hospitali ya **"Arusha Lutheran Medical Centre (ALMC)" saa 3.00 asubuhi (26.9.2025)** na litafungwa **Jumapili saa 10.00 jioni (28.9.2023)**. Wajumbe wa kulala wataondoka Jumatatu asubuhi **tarehe 29.9.2025.** Pia kumbuka kwamba yapo mabasi ya kusafiri usiku.

### KUTUMA PESA KWA SIMU:

TUMA KWA MTUNZA HAZINA HCF TAIFA (Tafadhali tuma fedha ya Kongamano na ya kutolea ukizingatia masharti ya mtandao utakaoutumia).

**M-Pesa: +255-764-753093 JINA: (Godwin Magwira);**
**Airtel-Money:+255-789-103391 JINA : (Godwin Magwira);**

### KUTUMA PESA MAKAO MAKUU YA HCF TANZANIA KUPITIA BENKI TAFADHALI ZINGATIA KUWAHI NAFASI KWA KUWAHI KULIPIA.

Nambari ya Akaunti ya HCF iko nyuma ya kipeperushi hiki. Tafadhali weka pesa za kujiandikisha/ ada yote ya kongamano katika akaunti ya NMB, kisha toa taarifa kamilifu kwa Mratibu (Ms. Maria Singano-Jalas) bila kuchelewa. Tafadhali kumbuka kuja na "Bank slip" kutoka benki ulikolipia yenye sahihi na muhuri wa benki husika. Tunaomba Viongozi wa HCF matawini kukusanya fedha za Wajumbe na kuzituma na majina yao kwa pamoja pale inapowezekana bila kuchelewa.